
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA





JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.19. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Aprili 1-10, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 11-20, 2023*

**MUHTASARI**


- Mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi ya nchi zitasaidia katika ukuaji wa mazao.
- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wanashauriwa kumalizia shughuli za kupanda mazao hususan yale yanayokoma haraka na kustahimili ukame wakifuata ushauri wa maafisa ugani
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanahimizwa kuzingatia taarifa za hali ya hewa kwa shughuli na mipango ya kila siku

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii iliendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikua juu ya wastani. Hali hii ilikua na mchango katika kutengeneza migandamizo midogo ya hewa sambamba na kueneza upepo wenye unyevunyevu kutoka mashariki na kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Kwa upande mwingine, joto la bahari katika upande wa mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) lilikua juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango katika kuusafirisha upepo wenye unyevunyevu wa magharibi kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Maeneo mengi ya nchi yamepata kiwango cha mvua kati ya mm 26 hadi 50. Kiasi cha cha mvua cha chini ya mm 26 kimeripotiwa katika maeneo machache ya mikoa ya Manyara, Dodoma, Ruvuma na Singida kama inavyoonekana katika Kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 1-10, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Katika kipindi cha dekadi iliyopita, mazao yameendelea vizuri kutokana na mvua za msimu zinazoendelea. Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa.

Kwa ujumla mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hatua ya kukomaa kwa mikoa ya Mbeya, Njombe, Songea, Rukwa, Iringa, Tabora na Kigoma. Aidha, zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hali ya kuridhisha.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kuchanua katika maeneo ya mikoa

ya Morogoro kusini, Tabora, Mbeya na Rukwa.

Kwa upande wa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wakulima wamendelea kupanda mazao kwa ajili ya msimu wa Masika.

Zao la viazi mviringo lipo katika katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya na baadhi ya wakulima wameendelea kuvuna zao hilo.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini kutokana na mvua zinazoendelea

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde viliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizonyesha.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia inatarajiwa kuongezeka nguvu na ile iliyopo katika kizio cha kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupunguza nguvu. Hali hii inatarajiwa kuuruhusu Ukanda mvua (ITCZ) uendelee kuambaa katika maeneo ya kaskazini. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani hali itakayopelekea kusafirishwa kwa hewa yenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani. Joto la bahari mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wa magharibi wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata vipindi vya ukavu.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utaendelea kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Msimu wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu maendeleo ya mazao mashambani na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wanashauriwa kumalizia shughuli za kupanda mazao hususan yale yanayokoma haraka na kustahimili ukame wakifuata ushauri wa maafisa ugani.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuongezeka kidogo kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.



Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)